TANGAZO LA SERIKALI NA. 428 la tarehe 17/6/2022

SHERIA YA FEDHA ZA UMMA,
(SURA YA 348)

# AMRI

*(Imetengenezwa chini ya kifungu cha 17 (1))*

AMRI YA UANZISHAJI WA MFUKO WA WAKALA WA BARABARA VIJIJINI NA MIJINI TANZANIA, 2022

## SEHEMU YA KWANZA
## MASHARTI YA UTANGULIZI

1. Jina.
2. Tafsiri.

## SEHEMU YA PILI
## UANZISHAJI WA MFUKO MAALUM

3. Uanzishaji.
4. Madhumuni ya Mfuko.
5. Majukumu ya Mfuko.
6. Usimamizi na uongozi wa Mfuko.
7. Vyanzo vya fedha.
8. Mgawanyo wa fedha.
9. Matumizi ya fedha.
10. Salio la ziada.
11. Mwaka wa fedha wa Mfuko.
12. Hesabu, ukaguzi na taarifa ya mwaka.

SHERIA YA FEDHA ZA UMMA,
(SURA YA 348)

**AMRI**

*(Imetengenezwa chini ya kifungu cha 17 (1))*

AMRI YA UANZISHAJI WA MFUKO WA WAKALA WA BARABARA VIJIJINI NA MIJINI TANZANIA, 2022

SEHEMU YA KWANZA
MASHARTI YA UTANGULIZI

Jina

1. Amri hii itajulikana kama Amri ya Uanzishaji wa Mfuko wa Wakala wa Barabara Vijijini na Mijini Tanzania, 2022.

Tafsiri

2. Katika Amri hii isipokuwa kama muktadha utahitaji vinginevyo-

Sura. 348

"Sheria" maana yake ni Sheria ya Fedha za Umma;

TS Na. 211 ya 2017

"Wakala" maana yake ni Wakala wa Barabara Vijijini na Mijini Tanzania iliyoanzishwa chini ya Amri ya Uanzishaji Wakala za Serikali (Wakala wa Barabara Vijijini na Mijini Tanzania), 2017;

TS Na. 211 ya 2017

"Mtendaji Mkuu" maana yake ni Afisa Mtendaji Mkuu wa Wakala wa Barabara Vijijini na Mijini Tanzania aliyeteuliwa kwa mujibu wa Amri ya Uanziahaji wa Wakala za Serikali (Wakala wa Barabara Vijijini na Mijini Tanzania), 2017;

"Mfuko" maana yake ni Mfuko wa Wakala wa Barabara Vijijini na Mijini Tanzania ulioanzishwa chini ya aya ya 3;

"Waziri" maana yake ni Waziri mwenye dhamana na masuala ya Wakala wa Barabara Mijini na Vijijini Tanzania; na

"Katibu Mkuu" maana yake ni Katibu Mkuu mwenye dhamana na masuala ya Wakala wa Barabara Mijini na Vijijini Tanzania.

## SEHEMU YA PILI
## UANZISHAJI WA MFUKO MAALUM

Uanzishaji

3. Unaanzishwa Mfuko Maalum utakaojulikana kama Mfuko wa Wakala wa Barabara Mijini na Vijijini Tanzania au kwa kifupi "MFUKO WA TARURA".

Madhumuni ya Mfuko

4. Madhumuni ya Mfuko yatakuwa ni-
(a) kukusanya rasilimali na kugharamia maendeleo na kukarabati mtandao wa barabara mijini na vijijini; na
(b) kukusanya rasilimali na kugharamia shughuli yoyote inayoendana moja kwa moja au inayohusiana na maendeleo na ukarabati wa mtandao wa barabara vijijini na mijini.

Majukumu ya Mfuko

5. Majukumu ya Mfuko yatakuwa ni kugharamia-
(a) maendeleo na matengenezo ya mtandao wa barabara vijijini na mijini;
(b) ukarabati na uboreshaji wa mtandao wa barabara vijijini na mijini;
(c) uanzishaji, ukarabati na uhuishaji wa mifumo ya usimamizi wa barabara;
(d) marekebisho ya dharura, uboreshaji wa viraka, ukarabati, uongezaji wa hadhi na ujenzi wa barabara;
(e) uboreshaji wa usalama wa barabara na usimamizi wa madhara ya mazingira katika mtandao wa barabara;
(f) uanzishaji na uendeshaji wa mizani na udhibiti wa uzito wa gari katika mtandao wa barabara vijijini na mijini;
(g) utoaji wa msaada wa kitaalam, usimamizi, uhakiki wa ubora na udhibiti kuhusiana na mtandao wa barabara vijijini na mijini;
(h) utengaji na ulinzi wa maeneo ya akiba ya barabara;
(i) ufanyaji wa utafiti kwa madhumuni ya kusaidia mpango wa Wakala wa shughuli za maendeleo na ukarabati; na

(j) shughuli za usimamizi, ufuatiliaji na shughuli nyingine zinazohusiana na kazi za barabara.

Usimamizi na uongozaji wa Mfuko

TS Na. 211 ya 2017

6. Mfuko utasimamiwa na kuongozwa na Mtendaji Mkuu ambaye atakuwa ni afisa masuuli wa Mfuko na idadi ya watumishi watakaoteuliwa au kupangiwa katika makundi mbalimbali kwa mujibu wa Amri ya Uanzishaji Wakala za Serikali (Wakala wa Barabara Vijijini na Mijini Tanzania), 2017.

Vyanzo vya fedha za Mfuko

TS Na. 211 ya 2017

7. Vyanzo vya fedha za Mfuko, vitakuwa ni pamoja na vyanzo vilivyoainishwa chini ya Amri ya Wakala za Serikali (Wakala wa Barabara za Vijijini na Mjini Tanzania) 2017, vikijumuisha-

(a) fedha kama zitakavyotengwa na Bunge kwa madhumuni ya Mfuko;

(b) ushuru wa barabara na mafuta uliowekwa kwenye petroli na dizeli na zilizotengwa kwa Wakala wa Barabara za Vijijini na Mjini kwa mujibu wa kifungu cha 4A cha Sheria ya Ushuru wa Barabara na Mafuta; na

Sura. 220

(c) kiasi kingine kutoka vyanzo vingine kama kitavyopokelewa na Mfuko.

Mgawanyo wa fedha

8.-(1) Fedha zilizowekwa katika Mfuko zitatumika katika kulipia miradi stahiki ya kipaumbele ya barabara.

(2) Bila kuathiri aya ndogo ya (1) fedha zitatengwa kwa namna ifuatayo-

(a) angalau asilimia tisini ya fedha zilizowekwa katika Mfuko zitatumika kwenye ujenzi wa barabara;

(b) sio zaidi ya asilimia tano ya fedha zilizowekwa katika Mfuko zitatumika kwa ujenzi wa dharura au haraka wa barabara kwa kibali cha Katibu Mkuu; na

(c) sio zaidi ya asilimia tano ya fedha zilizowekwa katika Mfuko zitatumika kwa ajili ya shughuli za kiutawala, ufuatiliaji na shughuli nyingine zinazohusiana na kazi za barabara.

Matumizi ya fedha

9.-(1) Katibu Mkuu atawajibika kuidhinisha Mpango Mkakati, Mpango wa Biashara na Bajeti ya Mwaka ya TARURA.

(2) Kwa madhumuni ya aya ndogo ya (1), matumizi hayataweza kufanyika isipokuwa chini ya mamlaka ya hati iliyotolewa na Katibu Mkuu mwenyewe kwenda kwa Mtendaji Mkuu.

(3) Hati chini ya aya hii haitatolewa kuhusiana na mwaka wowote wa fedha isipokuwa makadirio ya mapato na matumizi ya Mfuko kwa mwaka wa fedha yaliyoidhinishwa na Waziri yamewasilishwa mbele ya Bunge:

Isipokuwa kwamba, makadirio mengine ya mapato na matumizi ya Mfuko yaliyoidhinishwa na Katibu Mkuu na kuridhiwa na Waziri, ambayo mgao wake hauhitaji hati ya malipo, hautawasilishwa mbele ya Bunge.

Salio la ziada

10. Mapato, malimbikizo na fedha nyingine mwishoni wa mwaka wa fedha zitabaki katika Mfuko kwa madhumuni ya uanzishwaji wake.

Mwaka wa fedha wa Mfuko

11. Mwaka wa fedha wa Mfuko utakuwa ni kipindi cha mwaka mmoja unaoishia tarehe 30 Juni.

Hesabu,

12.-(1) Mtendaji Mkuu ndani ya miezi mitatu ya

ukaguzi na taarifa ya mwaka

mwisho wa kila mwaka wa fedha, ataandaa taarifa za fedha kwa kuzingatia Viwango vya Hesabu vya Kimataifa na Kanuni za Jumla za Hesabu zinazokubalika na kuridhiwa na Bodi ya Taifa ya Wahasibu na Wakaguzi.

(2) Hesabu zitaandaliwa kwa mujibu wa viwango vilivyotolewa na Bodi ya Taifa ya Wahasibu na Wakuguzi na zitasainiwa na Mtendaji Mkuu na kuwasilishwa kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali na nakala kwa Katibu Mkuu.

Dodoma,
10 Juni, 2022

MWIGULU LAMECK NCHEMBA MADELU
*Waziri wa Fedha na Mipango*